# Zifahamu athari za utupaji ovyo wa makopo ya viuatilifu

NA WARIOBA IGOMBE

UPO msemo usemao kuwa "Tunza mazingira yakutunze" msemo huo bado unaonekana kuwa haujaleta mafanikio kwani utupaji taka ovyo wa aina mbalimbali ikiwemo za plastiki kunaharibu taswira ya uhifadhi wa mazingira.

Miongoni mwa athari za utupaji taka za plastiki ni magonjwa mbalimbali yakiwemo ya saratani, pia taka hizo huchangia kwa kiasi kukubwa kuchafua vyanzo vya maji ikiwa pamoja na kuchafua kwa kiasi kikubwa maji ya baharini na maziwa.

Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzuguka mwanadamu na viumbe hai katika maisha yao, hivyo kila tunachokiona ni mazingira ambapo mazingira yakiwa katika hali ya usafi hupendeza na kuvutia.

Mazingira yasipowekwa katika hali ya usafi huhatarisha afya ya viumbe hai waishio katika mazingira hayo ikiwemo binadamu, wanyama,na mimea.

Pamoja na serikali kutangaza kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilifungwa rasmi Mei 31, 2019, bado kumekua na changamoto ya watu kutupa makopo ya plastiki holela katika maeneo mbali mbali ya jamii zetu hapa nchini.

Hali hii inahatarisha sana afya ya mazingira kwani makopo hayo huokotwa na watoto au watu wazima,wakati mwingine bila kufahamu makopo hayo yalitumika kuweka kimiminika cha aina gani.Makala haya yamelenga inaelezea madhara ya utupaji holela wa makopo yaliokwisha matumizi ya viuatilifu.

Meneja wa Taasisi Kuendeleza Kilimo hapa nchini(SAGCOT),John Nakei ni kuwa utupaji ovyo makopo ya viuatilifu yalivyokwisha kutumika niuharibufu mkubwa wa mazingira.

Nakei alieleza mbali na utupaji ovyo wa vifuhashio vya viuatilifu ikiwemo makopo ya plastiki kuwa ni miongoni mwa uharibifu mkubwa wa mazingira vilevile utupaji huo kunaweza kusababisha madhara kwa jamii hapa nchini.

Alisema baada ya matumizi ya viuatilifu, baadhi ya watumiaji hususan wakulima na wafugaji hutupa makopo maeneo yasiyo sahihi ambapo watu wengine wakiwemo watoto huyaokota na kuanza kuyachezea.



Baadhi ya vijana wanaounda kikundi cha uhamasishaji wa utunzaji mazingira mkoani Morogoro, wakisafisha mto Morogoro uliopo Manispasaa ya Morogoro, kwa kuondoa chupa za plastiki.

Alisema baadhi ya kina mama pia huyatumia kwa matumizi mengine ya nyumbani kama vile kuweka chumvi, sukari au vimiminika kama vile maji au maziwa jambo ambalo ni hatari kwa afya ya mtumiaji.

Meneja huyo alisema kitendo hicho kinahatarisha usalama wa watu na kuepukana na tatizo hilo, wauzaji wa viuatilifu wanatakiwa kabla ya kuuza bidhaa wanatakiwa kutoa elimu kwa wateja.

"Kwetu sisi tumekuwa tukiotoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu baada ya matumizi ambapo tumekuwa tukiwamiza wakulima kujenga vizimba shambani ili chupa zote na vifungashio vya viuatilifu baada ya matumizi viweke sehemu sahihi ili baadaye uchafu huo uchome" alisema Nakei.

Alisema mbali na watu kuokota makopo hayo kwa ajili ya matumizi mengine ya nyumbani ikiwemo watoto kuyachezea bila kujali athari zinazoweza kutokea utupaji ovyo wa makopo hayo ya vifungashio vya viuatilifu husababisha kwenda katika vyanzo vya maji.

Natei alisema suala hilo ni mtambuka hivyo kila mtu anatakiwa kulitazama kwa jicho la tatu kuepuka athari zinazoweza kutokea, amewapongeza wadau wa mazingira ikiwemo Taasisi ya HUDEFO kwa mikakati yake ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira utokanao na taka za plastiki.

Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzuguka mwanadamu na viumbe hai katika maisha yao, hivyo kila tunachokiona ni mazingira ambapo mazingira yakiwa katika hali ya usafi hupendeza na kuvutia. Mazingira yasipowekwa katika hali ya usafi huhatarisha afya ya viumbe hai waishio katika mazingira hayo ikiwemo binadamu, wanyama,na mimea. Pamoja na serikali kutangaza kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilifungwa rasmi Mei 31, 2019, bado kumekua na changamoto ya watu kutupa makopo ya plastiki holela katika maeneo mbali mbali ya jamii zetu hapa nchini.

## VIUATILIFU

Viuatilifu ni sumu ambayo hutumika kuua,kuangamiza,kufukuza,au kuzuia visumbufu katika mimea.Visumbufu vya mimea vinaweza kuwa wadudu, kuvu (fangasi),magugu, pamoja na baadhi ya wanyama na ndege.

Kituo cha Utafiti wa Viuatilifu cha TPRI (Tropical Pesticide Research Institute) kimekuwa kinafanya tafiti na kinatoa mafunzo na huduma katika afya ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira juu ya athari za matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu.

Mkuu wa Kitengo cha UdhibitiwaViuatilifunaUtunzaji wa Mazingira,TPRIMwema Felix alitoa ushauri kwa jamii hususani wakulima wanaotumia viuatilifu kutokuvitupa holela vifaa vinavyotumika kutunzia viuatilifu baada ya kuvitumia.

Utupaji holela wa makopo vya plastiki

Felix alisema kwamba viuatilifu vingi baada ya kutengenezwa viwandani huifadhiwa katika makopo au mifuko ya plastiki au chupa na huwa na maelezo kuhusu kimiminika ama kiuatilifu hicho.

"Watu wengi hasa baadhi ya wakulima wamekua wakitupa holela baada ya kumaliza matumizi yake.Baadhi ya vitunzio hivyo kama makopo au vifuko vya plastiki vimekua vikirushwa katika vyanzo vya maji ambayo hutumiwa kwa matumizi ya binadamu na hata wanyama pia"alisema Felix.

Kutokana na kushamiri kwa biashara za makopo ya plastiki katika maeneo mengi vijana wengi kutokana na ugumu wa maisha lakini pia watoto wa shule wamekua wakitembea na kuokota makopo ya plastiki ili kujipatia kipato.

Mbali na kwamba uokotaji wa makopo haya ya plastiki inasemekana umesaidia kupunguza uzagaaji wa makopo hayo katika jamii,ni dhahiri kwamba ukusanyaji wa makopo hauzingatii afya ya muokotaji.

Katika maeneo mengi usalama wa vyanzo vya maji umekua katika hatari ya kuathiriwa kutokana na utupaji holela wa vifaa vilivyotumika kutunzia vimiminika vyenye kemikali zenye sumu kama viuatilifu au mbolea za viwandani.

Kemikali hizo kwa kawaida hazionekani kwa macho na ni vigumu kuzigundua hivyo maji yanapaswa kupimwa kwenye maabara kuchunguza uwezekano wa kuwepo sumu au kemikali za viwandani.

Felix alisema kwamba taasisi ya TPRI imekua ikifanya na inaendelea kufanya chunguzi huu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili hukakikisha jamii inapata elimu itakayosaidia sana ekupukana na athari zinazoweza kusababishwa na utupaji ovyo wa makopo ya plastiki ambayo ni vifungashio vya viuatilifu.

Alisema maji yaliochafuliwa huweza kuwa na mabaki ya viuatilifu ambavyo huweza kumuathiri binadamu atumiapo maji hayo na madhara haya kwa kawaida huonekana haraka kwa wazee na watoto kwani wao huwa na kinga ya mwili (immunity) ndogo.

Felix alisema kwa wanyama hutumia kiasi kikubwa cha maji hivyo pindi wanapokunywa maji yale yenye mchanganyiko wa kemikali hizo za viuatilifu maji hayo huweza kuharibu homoni za kike na kiume na vina saba na kuna hatari ya kusababisha mnyama kuzaa kiumbe ambacho hakijakamilika.

Kwa upande wa mimea, Felix alisema huathirika kutokana na kunyonya kemikali hizo na baadae hufa ambapo mimea hiyo inaweza kuwa ni chakula au hutumika kama hifadhi kwa wanyama waishio katika maji na inaathirika na kufa.

Udongo nao huathirika kwa kemikali hufyonzwa katika udongo na kuua wadudu ambao ni rafiki wa mazingira na muhimu katika urutubishaji wa udongo ambapo wadudu kama minyoo, konokono, mchwa na hata vyura ambao huitajika katika ikolojia ya eneo hilo hufa.

## NEMC

Naye, Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazinrira nchini(NEMC) mkoa wa Morogoro, Abel Sembeka alisema sheria ya mazingira ya mwaka 2004 inakataza uchafunzi wa mazingira wa aina yoyote.

Sembeka alisema kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ya mwaka 2021 ni kuwa suala la utunzaji mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji ni la kila mtu hivyo ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinalindwa ipasavyo.

"Katiba ya nchi yetu inasema kujumu la kutunza mazingira ni la kila mtu,utupaji ovyo wa taka kwenye mito,vyanzo vya maji ni ukiukwaji wa sheria kwa mjibu wa katiba kwa hiyo wote wanafanya hivyo wanatakiwa kuacha kabla sheria haijachua mkondo" alisema Sembeka.

Nini kifanyanyike kuzuia utupaji holela makopo ya viuatilifu

Daktari bingwa wa magonjwa ya ndani kutoka Hospitali ya Rufaa mkoa wa Morogoro Clement Lubeya alisema kwamba njia pekee ya kuzuia utupaji wa makopo ya plastiki holela ni kuihamasisha jamii,kutenga maeneo kwaajili ya kutupa makopo hayo ya plastiki yaliyokua na viuatilifu.

Alisema kwamba kabla ya kutupa chupa iliyokwisha kiuatilifu unatakiwa kuisuuza kwa maji mengi mara tatu na baada ya hapo kuiharibu kwa kuitoboa ili isiweze kutumika tena kisha kuipeleka katika eneo la kukusanyia chupa hizo.

Dk. Lubeya alisema kuwa utumiaji viuatilifu kwa njia isiyo sahihi pia kunahatarisha afya ya mtumiaji na kwamba watumiaji wote wanatakiwa kuzingatia sauala la afya kama vile kuvaa gloves kabla na baada ya kumuliza kazi na hata wakati wa kuosha kopo au chupa iliyokwisha kiuatilifu.

"Ili kulinda maji yasichafuliwe na kemikali zenye sumu za viuatilifu ni vizuri kuzuia uchafuzi kwenye vyanzo vya maji hivyo jamii inatakiwa kuelimishwa juu ya hili ikiwa ni pamoja na athari za utupaji wa vifungashio vya aina mbalimbali"anasema Lubeya.

Alisema yapo madhara mengi ambayo yanaweza kumpata binadamu asiponzingatia utumiaji na uhifadhi mzuri wa vifungashio vya viuatilifu kuwa ni pamoja naafya kudhorota,tumbo kuuma,kuharisha,kuharibu mfumo wa damu,huathiri ini na mengineyo pamoja na magonjwa ya saratani.

Dk. Lubeya alitoa ushauri hasa kwa wakulima kutumia njia za asili za kuzuia wadudu na mbolea za asili (mboji) badala ya kemikali zenye sumu kwani kutasaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa madhara yatokanayo na matumizi ya viuatilifu au mbolea za viwandani.

Stephen Same ni Ofisa Kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, alisema elimu kuhusu vifaa kinga kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuweza sehemu sahihi vifungashio vya viuatilifu imekuwa ikilolewa mara kwa mara lakini baadhi ya wakulima wamekuwa wahafuati mashariti ya wataalamu.




Makopo ya plastiki yaliyokuwa na viuatilifu yakiwa yametupwa shamba baada ya matumizi.

"
Daktari bingwa wa magonjwa ya ndani kutoka Hospitali ya Rufaa mkoa wa Morogoro Clement Lubeya alisema kwamba njia pekee ya kuzuia utupaji wa makopo ya plastiki holela ni kuihamasisha jamii,kutenga maeneo kwaajili ya kutupa makopo hayo ya plastiki yaliyokua na viuatilifu.

"Elimu imekuwa ikitolewa kwa wakulima wengi suala hili hawalipi uzito na ndiyo sababu ya kuendea kwa makopo ya plasitiki na vifungashio vingine vya viuatilifu mitaani hali inayopelea kuchafua mazingira pamoja na vyanzo vya maji"alisema Same.

Kwa upande muuzaji na msambazaji wa pembejeo,Prisca John anasema wamekuwa wakiwashauri sana wakulima namna ya matumzi sahihi ya viuatilifu kabla na baada ya matumizi lakini kwa kuwa wengi wao wanalima kikimo cha mazoea suala hilo limekuwa ni gumu kutekelezeka.

Amos Lucas mkulima na Sarah Tomas ambaye ni mfugaji mkoani Morogoro wanakiri kuyatupa ovyo makopo ya plastiki baada ya matumizi ya viuatilifu na kwamba wamekuwa wakifanya hivyo kutokana na kutokuwa na elimu ambapo wamewaomba wadau kuendelea kutoa elimu hiyo zaidi kwa jamii nchini.



Kizimba cha kuhifadhia chupa za plastiki na vifungashio vingine vya viuatilifu baada ya matumizi.